

WATEULE TUSIFADHAIKE KABISA

NDANI YA MIOYO YETU

MAANDIKO : YOH. 14: 1 – 4.

1. UTANGULIZI

Yesu baada ya kuiona mioyo ya wanafunzi wake imefadhaika kwa sababu aliwaambia katika sura ya **13** kwamba anawaacha; aliwaambia neno hili muhimu sana la matumaini kwamba wasifadhaike mioyoni mwao maadamu tayari wamemwamini Mungu. Yesu anafahamu fika kwamba katika kila maisha ya mtu aliyemwamini yeye kuna wakati yatatokea mambo magumu yatakayofadhaisha moyo wake; lakini anatutaka tusifadhaike kama watu wasiomwamini Mungu, bali katika mambo hayo yote tumtegemee Mungu na kumtwisha mizigo yetu.

- Katika maisha haya ndugu zangu nimejifunza kwamba kuna **“nyakati nyingine ngumu ambazo zinapopita juu yetu; tunakuwa hatuna budi kuzikubali maadamu liko kusudi la Mungu la kuruhusu tuzipitie chini ya jua, Mhub. 3: 1 – 8, na kazi yetu kubwa katika nyakati kama hizi ni kujikabidhi kwa Mungu tu. Zab. 31: 3, 15.**
- Katika kusoma Biblia nimegundua kwamba nyakati nyingine zinamtoka mtu katika maisha yake baada ya kuokoka ili kupima uhalisia wa imani yake kwa Mungu kama tunavyojifunza juu ya Daniel na wenzake, **Mordekai, Yusufu, Esta na wengine wengi**; lakini pia nyakati nyingine zinaweza zikatoka katika maisha ya wateule wengi ili kupembua ngano na pumba katika Kanisa la Bwana. **Waam. 7: 1 – 8, Luk. 22: 28- 34.**

Note: Saa yote na wakati wote tunapokuwa tunapitia katika hali tofauti tofauti ngumu na za baraka, Yesu anakuwa anaisoma mioyo yetu jinsi ilivyo mbele zake; Huwezi kufahamika jinsi ulivyo moyoni hadi changamoto

zinaporuhusiwa kupita juu ya maisha yako. Ayub. 2: 9 -10, Ruth. 1: 8 – 18, Hesab. 14: 1 – 9. n.k.

2. Yesu alipowaambia wanafunzi wake neno hili msifadhaike mioyoni mwenu maana yake:-

a. Ndani yao aliona mahangaiko ya mioyo yao pamoja na maswali mengi wanayojijibu wao wenyewe; akaona jinsi walivyovaliwa na roho ya wasiwasi na usumbufu mwingi katika akili zao bila majibu. **Hes. 13: 25 – 33, 14: 1 – 4, 1Samwl. 17: 1 – 11, Kut. 14: 10 – 14.**

b. Ndani yao Yesu aliona jinsi walivyokosa furaha, amani pamoja na changamko la moyo ambalo walikuwa nao muda wote walipokuwa wanatembea naye. **Yoh. 13: 36 – 37.**
“Na mojawapo ya silaha kabambe ya shetani kwa Kanisa la Mungu ni kuleta vitisho kwa mambo mabaya yatakayowapata ili wakate tamaa na kufadhaika daima.

3. Dawa ya kushinda fadhaa ya aina yoyote Yesu aliisema **“Tumwamini Mungu kwamba hili nalo anaweza, hili nalo litapita. Zab. 107: 20, 2Kor. 10: 3 – 5, 2Nyakt. 32: 7 -8, 1Samwl. 17: 31 – 37; Mt. 11: 28 – 29**

- Kwa lugha nyingine Yesu alipowaambia kuwa wasifadhaike mioyoni mwao – alitaka waangushe mawazo mabovu ya woga; wasiwasi pamoja na mahangaiko waliyokuwa nayo na wamwamini Mungu kuwa anaweza.

4. Nimelazimika kufundisha eneo hili la kufadhaika kwa sababu kuna zaidi ya aina 800 ambazo zinasababisha mteule kufadhaika na kisha kuishi bila furaha wala amani wakati ameokoka; mojawapo ni pale mtu anapopitia katika hali ya **magonjwa mabaya na yanayotisha; uchumi wa mtu kuporomoka ghafla, watoto kuharibika, kubakwa, kukataliwa, umaskini, kukosa ajira; kufiwa na mpendwa wako; kufukuzwa kazi, kushindwa masomo, kudhulumwa na wapendwa, kushambuliwa na majambazi, kuharibu mimba au kutoshika mimba kabisa (ugumba) kukosa nguvu za**

kiume na mengine mengi; yote haya shetani anaweza akayatumia kama silaha yake ya kutisha wateule wa Mungu ikiwa ni pamoja na waume kuacha wake zao na kuoa wengine au kuhamia nyumba ndogo; yote haya kama tutamwamini Mungu jibu lipo kwake na yanatatulika.

- **Kitabibu: Mtu aliye na fadhaa nyingi moyoni mwake; lazima atasumbuliwa na shinikizo la moyo mara kwa mara, kisukari, vidonda vya tumbo, maumivu ya kichwa sana, anakosa usingizi, anasumbuliwa na mawazo mabaya daima (anapoteza nia njema) amejaa wasiwasi na mashaka wakati wote n.k. yaani fadhaa ni mashambulizi kamili ya ibilishi kwa watoto wa Mungu, na bila msaada wa Mungu hata wateule wakati mwingine wanakata tamaa na hata kuanza kujiombea maombi mabaya. 1Wafal. 19: 1 – 10, Mdo. 5: 17 – 21, Mdo. 12: 1 – 12.**
- Ndiyo sababu Yesu alipokutana na wanafunzi wake wamejaa fadhaa moyoni mwao, hakuwashambulia kwa maneno makali bali aliwaelekeza njia; na njia nyingine iliyo bora zaidi saa ya mambo magumu ni kuimba tenzi za Rohoni pamoja na kumsifu Mungu. **Yak. 5: 13, Kolos. 3: 16.**

MWISHO

Katika ibada hii, Yesu anatuona sote jinsi tulivyo mbele zake, tuweke kando yote yanayotufadhaisha, na tumwamini Mungu kwamba hata hili anaweza kutuvusha na litapita; katika Jina la Yesu. **Amina.**

Na

Askofu Dr. L. M. Mwizarubi

27/03/2022